# KWA BWANA KUNA FADHILI

Wimbo wa Katikati Dominika ya 5 ya Kwaresma Mwaka A

Na. Aloyce G. Msafi
Harmony na Kassian F
Kiomboi Parish
22.03.2020

**Zaburi 130 (K) 7**




1. Ee Bwana, toka vilindini nimekulilia/
   Bwana, uisikie sauti yangu./
   Masikio yako na yaisikilize/
   Sauti ya dua zangu.

2. Bwana, kama Wewe ungehesabu maovu, /
   Ee Bwana, nani angesimama? /
   Lakini kwako kuna msamaha/
   Ili Wewe uogopwe.

3. Nimemngoja Bwana,/
   roho yangu imemngoja,/
   Na neno lake nimelitumainia.

4. Nafsi yangu inamngoja Bwana,/
   Kuliko walinzi waingojavyo asubuhi,/
   Naam, walinzi waingojavyo asubuhi,/
   Ee Israeli, umtarajie Bwana.

5. Maana kwa Bwana kuna fadhili,/
   Na kwake kuna ukombozi mwingi./
   Yeye atamkomboa Israeli/
   Na maovu yake yote.